# MTIHANI WA MUHULA KATI 2018

# DARASA LA TANO

# KISWAHILI: LUGHA

*Muda: Saa 1 dak 40*

**Chagua jibu sahihi ujaze nafasi zilizoachwa wazi kutoka nambari 1-15**

Visa ___1___ watu kudanganywa na___2____ yao kuchukuliwa huwahusu ___3___ watu wazima. _____4____ya watu _____5_____ ni watu walioelimika__6___ na kwa _____7____mtu akisikia kwamba mtu____8_____ huyo amedanganywa _____9____ walaghai na mali yake kuporwa, ni _____10____sana kuamini.

Hivi majuzi kumekuwa na visa ___11___ vya watu ___12___na watu wasiokuwa na silaha ____13____ isipokuwa ulimi ___14___mtamu. Walaghai humfanya watu kupoteza pesa___15___ sana.

1. A. ya B. za C. vya D. wa
2. A. viti B. mali C. watoto D. shamba
3. A. lakini B. ingawa C. isipokuwa D. hasa
4. A. Baadhi B. Wengi C. Wachache D. Miongoni
5. A. anayedanganywa B. wanayedanganywa C. wanaodanganywa D. anaodanganywa
6. A. jinsi B. hivi C. kama D. sana
7. A. hivyo B. hicho C. huu D. hiyo
8. A. hadi B. kama C. hio D. ili
9. A. pengine B. akiwa C. na D. ila
10. A. ilivyo B. ndefu C. juu D. vigumu
11. A. vingi B. kingi C. mingi D.wengi
12. A. aliyelaghaiwa B. waliolaghaiwa C. uliolaghaiwa D. zilizolaghaiwa
13. A. wowote B. lolote C. chochote D. yoyote
14. A. wao B. yao C. lao D. zao
15. A. mingi B. nyingi C. mengi D. kingi

***Kuanzia nambari 16-30, jibu swali kulingana na maagizo***

16. **Kanusha sentensi:**
Mgeni ameenda sebuleni.
   A. Mgeni hakuenda sebuleni
   B. Mgeni hataenda sebuleni
   C. Mgeni hajaenda sebuleni
   D. Mgeni haendi sebuleni

17. Makao ya kuku ni
   A. kizimbani
   B. tundu
   C. kombe
   D. kichuguu

18. **Tumia -ingine:**
Amenunua gari____________
   A. nyingine
   B. lingine
   C. jingine
   D. ingine

19. Mtoto wa mjomba au shangazi ni
   A. mpwa
   B. binamu
   C. halati
   D. kitukuu

20. Neno, **'Kipepeo'** liko katika ngeli gani?
   A. U-I
   B. I-ZI
   C. KI-VI
   D. A-WA

21. Kifaa kinachotumiwa kukunia nazi huitwaje?
   A. Mbuzi
   B. Seredani
   C. Kinu
   D. Sinia

22. **Kamilisha sentensi:**
Alifika mapema___hakumpata.
   A. ili
   B. lakini
   C. hata
   D. hadi

23. Kinyume cha neno '**giza**' ni
   A. jua
   B. nyeupe
   C. mchana
   D. mwangaza


24. **Chagua wingi wa:**
Karatasi hii imeraruka.
   A. Makaratasi haya yameanguka
   B. Makaratasi hizi zimeraruka
   C. Karatasi hizi zimeraruka
   D. Karatasi hizi imeraruka

25. **Kamilisha methali:**
Mgema akisifiwa__
   A. huvunjika guu
   B. hali wali mkavu
   C. hula mbivu
   D. tembo hulitia maji

26. Akisami $^1/_5$ kwa maneno ni
   A. thuluthi
   B. sudusi
   C. robo
   D. humusi

27. Gani kati ya viumbe hawa ni ndege?
   A. Kanga
   B. Pundamilia
   C. Chui
   D. Kupe

28. Umbo hili ni gani?



   A. Mraba
   B. Mche
   C. Pia
   D. Mstatili

29. **Kamilisha sentensi:** Wanafunzi ______ walituzwa.
   A. wasafi
   B. wasita
   C. wahodari
   D. safi

30. **Tumia -enye kwa usahihi**
Mti _____ matunda umekauka.
   A. yenye
   B. lenye
   C. wenye
   D. chenye

***Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40.***

Katika kijiji cha Mlachake, paliishi simba. Siku moja alihisi njaa sana. Akaamua kuenda kuwinda. Katika pitapita zake za kuwinda, alimkuta sungura akiwa amelala fofofo. Alishusha pumzi, akatabasamu na kumshukuru sana Mungu kwa ukarimu wake wa kutambua taabiko lake na kumtunuku chakula pasi na haja ya kukitolea jasho.

Taratibu alimsogelea sungura ili asije akamwamsha. Alipoinua miguu yake kutaka kumkamata, mara akatokea paa mnono ambaye alipita akikimbia karibu naye, akielekea upande wa kaskazini kwenye uwanda wa nyasi fupi.

Simba alimwacha sungura na akaanza kumkimbiza yule paa. Vishindo, kelele na purukushani za simba na paa vilimgutusha na kumwamsha sungura ambaye aliamka na kutimua mbio kuelekea upande wa kusini.

Baada ya kumkimbiza paa kwa muda mrefu, simba alishindwa kumkamata na akaamua kurudi ili akamle yule sungura. Alipogundua kuwa sungura naye alikuwa ameamka na kukimbia, simba alijilaumu na kusema. "Ama kweli, nimepata nilichostahili. Nilikiacha chakula nilichokitia mkononi tayari kwa tamaa ya kutaka kupata zaidi."

31. Simba aliamua kuenda kuwinda kwa sababu
    A. alikuwa mgonjwa
    B. alikuwa mvuvi
    C. alikuwa na wageni
    D. alihisi njaa
32. Simba alimkuta sungura akifanya nini?
    A. Akipika
    B. Akilala
    C. Akifua
    D. Akicheka
33. Simba aliishi katika kijiji cha
    A. Mlachake
    B. Heko
    C. Pwani
    D. Zawadi
34. Simba alimshukuru nani?
    A. Sungura
    B. Simba
    C. Mungu
    D. Ndovu
35. Mnyama yupi alipita akikimbia?
    A. Kobe
    B. Twiga
    C. Nyani
    D. Paa
36. Paa alikuwa akielekea upande wa
    A. Magharibi
    B. Kusini
    C. Kaskazini
    D. Mashariki
37. Sungura aliamshwa na
    A. upepo mkali
    B. mvua iliyokuwa ikinyesha
    C. mti ulioanguka
    D. vishindo, kelele na purukushani za simba na paa.
38. Sungura alipoamka alitimua mbio kuelekea
    A. Kusini
    B. Mashariki
    C. Kaskazini
    D. Magharibi
39. Simba alimkamata mnyama yupi?
    A. Paa
    B. Sungura
    C. Hakukamata mnyama yeyote
    D. Kondoo
40. Chagua kichwa mwafaka cha hadithi hii
    A. Sungura ashikwa na simba
    B. Simba mwenye tamaa
    C. Paa na sungura
    D. Mfalme wa wanyama

**_Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50_**

Kashata ni aina ya peremende au unaweza kuiita nusu biskuti. Ni aina ya kitafunio kilichoungwa kwa sukari nyingi. Kuna aina nyingi za kashata lakini zilizo maarufu ni kashata za machicha na kashata za karanga.

Mara nyingi sana utaona <u>wazee</u> nyakati za asubuhi au jioni wakicheza bao au karata wakinywa kahawa na kutafuna kashata. Wazee hawa hunywa kahawa nyeusi isiyokuwa na sukari. Hii ni kwa sababu kashata huwa ni tamu kwa sababu imeungwa na sukari nyingi.

Watoto nao hupenda sana kula kashata matembezeni au hata shuleni. Moja ya biashara ndogondogo ambazo kina mama hufanya ni ya uuzaji wa kashata. Uuzaji wa kashata huwa rahisi pahali kuna watoto wengi na wazee ambao hukaa vikundi vikundi wakicheza bao au karata. Kashata vilevile hupendeza sana zikiandaliwa kama aina moja ya vitafunio vilivyoandaliwa katika tafrija au sherehe au sikukuu ya aina fulani.

41. Kashata ni aina ya
    A. tunda
    B. mmea
    C. peremende
    D. ua
42. Kashata huungwa kwa
    A. chumvi
    B. sukari
    C. kitunguu
    D. nyama
43. Aina za kashata zilizo maarufu ni ngapi?
    A. Mbili
    B. Kumi
    C. Sita
    D. Tatu
44. Kinyume cha neno **wazee** ni
    A. wazazi
    B. wasichana
    C. wageni
    D. vijana
45. Wazee hunywa kahawa yenye rangi gani?
    A. Kahawia
    B. Nyeupe
    C. Nyeusi
    D. nyekundu
46. Wazee hutafuna kashata na kunywa kahawa wakicheza michezo gani?
    A. Kandanda au Karata
    B. Karata au Bao
    C. Bao au Kandanda
    D. Riadha au Kandanda
47. Watu ambao hupenda kula kashata wakiwa matembezeni au shuleni ni
    A. walimu
    B. wazazi
    C. wapishi
    D. watoto
48. Biashara ya uuzaji wa kashata hufanywa na
    A. akina mama
    B. vijana
    C. wanaume
    D. watoto
49. Kulingana na habari, kashata ni
    A. sharubati
    B. kinywaji
    C. kitafunio
    D. uji
50. Chagua kichwa sahihi cha habari uliyoisoma
    A. Unywaji wa kahawa
    B. Biashara ndogondogo
    C. Michezo ya wazee
    D. Kashata